Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki Iwe shauku

Toleo Na. 012 | Jarida la kila miezi mitatu | Oktoba - Disemba, 2012

## ZLSC Yasherehekea Kutimiza Miaka 20

SHEREHE kubwa zilizohudhuriwa na wawakilishi kutoka taasisi zilizopo ndani na nje ya Zanzibar zilifanyika Pemba Novemba 30, 2012 kushangilia Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kutimiza miaka 20 tokea kuanzishwa mwaka 1992.

ZLSC ilianzishwa mwezi Mei 1992 chini ya Sheria ya Land Perpetual Succession. Baadaye ZLSC ilisajiliwa chini ya Sheria ya Taasisi zisizo za Serikali, Societies Act, 1995, (Act No. 6 ya 1995).

Wanasheria waandamizi watatu walioanzisha ZLSC ni marehemu Profesa Haroub Miraji Othman (alifariki mwaka 2009), Maalim Hassan Said Mzee na Bibi Fatma Maghimbi (ambaye alijiuzulu baada ya kujiunga na siasa) .




*Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania , Mheshimiwa Barnabas Albert Samatta (mwenye suti nyeusi aliyekaa mstari wa pili kutoka mbele) ambaye alikuwa mgeni maalum katika kongamano la Wasaidizi wa Sheria lililofanyika katika ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund, Tibirinzi, Chake Chake, Pemba katika picha ya pamoja na washiriki. Sambamba na Kongamano hilo, ZLSC ilisherehekea miaka 20.*

Baadhi ya wageni maarufu waliohudhuria sherehe hizo zilizotanguliwa na Kongamano la siku mbili la wasaidizi wa sheria kutoka Unguja na Pemba alikuwa na Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mheshimiwa Barnarbas Samatta.

Mheshimiwa Samatta pia alifungua kongamano la wasaidizi wa sheria na kuwakabidhi vyeti wasaidizi wa sheria 54 waliohitimu masomo ya sheria ya awali ya miaka miwili yaliyofanywa na ZLSC.

Inaendelea Uk. 3

## Jaji Mkuu Mstaafu Aipongeza ZLSC Kutetea Haki za Wanyonge

- ***Vyombo vya Sheria Visiwe Vibogoyo***

JAJI Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta amekipongeza Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa mafanikio makubwa ya kutoa msaada wa sheria bila ya malipo kwa wanyonge ili wapate haki zao.

Mheshimiwa Jaji Mkuu Mstaafu alitoa pongezi hizo katika hotuba yake makhsusi *(keynote address)* aliyoitoa katika kongamano la wasaidizi wa sheria lililofanyika Novemba 30 hadi Disemba 01, 2012 katika ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund (ZSSF) uliopo Chake Chake, Pemba.

"Mnastahili pongezi sana. Mafanikio ya Kituo ni mengi sana katika miaka 20," alisema Mheshimiwa Jaji Samatta.

Aliyataja mafanikio ya ZLSC kuwa ni kutoa huduma mbali mbali za sheria kwa wanyonge, kutoa machapisho mbali mbali ya sheria, Ripoti ya Haki za Binadamu, Zanzibar, Maendeleo ya Katiba na Mafunzo ya Wasaidizi wa Sheria.

Alisema ZLSC imetetea haki za binadamu kwa kiwango ambacho kimewavutia watu wengi sana na

Inaendelea Uk. 3

### YALIYOMO

Toeni Maoni ya Katiba Bila ya Woga - Mwanasheria Mkuu Uk. 3

Wasaidizi wa Sheria Wahitimu Wapewa Vyeti Uk. 5

Uendeshaji wa Kesi ya Jinai Uk. 12

Tanzania Bado Haijafuta Adhabu ya Kifo Uk. 18

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri**
Prof. Chris Maina Peter

**Mwenyekiti**
Bi. Harusi Miraji Mpatani

**Wajumbe**
Bw. Ali Ahmed Uki
Bi. Safia Masoud Khamis
Bi. Jina Mwinyi Waziri
Bi. Farhat Rashid Omar

**Msanifu**
Aziz Iddi Suwed


**Ifanye haki**



**Iwe shauku**


Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:-

S.L.P: 3360 Zanzibar
Simu: +255-24-2233784
Fax: +255-24-223495
Email:info@zlsc.or.tz
Website:www.zlsc.or.tz

Chake Chake Pemba wasiliana nasi kwa:-
Simu: +255 24 2452936


Wananchi wote mnaombwa kusoma Jarida hili la Kituo kwa madhumuni ya kujifunza zaidi na kupima maendeleo ya utendaji kazi za Kituo

Tunakaribisha barua za maoni kutoka kwa wasomaji na michango ya makala kwa ajili ya kuelimisha umma

Aidha wale wote watakaopenda kuchangia au kuleta maoni yao watatakiwa kujitambulisha kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwazi katika kuendeleza Jarida hili.

Bodi ya Wahariri itakuwa na uwezo wa mwisho wa kuamua au kuhariri habari itakayochapishwa kwenye Jarida hili.

Mhariri.

## Maoni ya Mhariri

# ZLSC Yatimiza Miaka 20 ya Uhai



KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kilichoanzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha haki inapatikana *(access to justice)*, kutetea haki za binadamu, kutoa elimu ya sheria na kutoa machapisho ya sheria kimetimiza miaka 20 tokea kuanzishwa mwaka 1992.

ZLSC imeanzishwa chini ya waasisi na wadhamini watatu wa Bodi ya Wadhamini; marehemu Profesa Haroub Miraji Othman aliyefariki dunia mwaka 2009, Maalim Hassan Said Mzee na Bibi Fatma Maghimbi aliyestaafu mwaka 1995 baada ya kujiunga na siasa. Maadili ya ZLSC ni kwamba yoyote, bila ya kujali wadhifa wake, analazimika kujiuzulu anapojiunga na siasa ili kujenga imani kwa jamii.

Miaka 20 ya uhai wa ZLSC ni jambo la kujivunia sana kwa wote wanaopenda kuona haki ikisimama bila ya kujali tofauti zozote za binadamu zilizopo katika jamii. Aidha, miaka 20 ni kipimo tosha cha utendaji kazi na mafanikio ya ZLSC.

ZLSC imetoa machapisho kadhaa ya kitaalamu ya sheria, imeendesha semina na makongamano ya kitaaluma, imeendesha vipindi vya redio na televisheni vya sheria, inachapisha Ripoti ya Haki za Binadamu Zanzibar kila mwaka na kuchapisha Jarida kila baada ya miezi mitatu.

Wale wote wanaoifahamu historia ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ya Zanzibar watakubaliana na ukweli kwamba haikuwa kazi nyepesi hata kidogo ZLSC kudumu kwa miaka 20. Mawimbi makubwa na madogo yalijaribu kutikisa uhai wake katika nyakati tofauti hususan mwaka 1995 hadi mwaka 2000.

Lakini ngome imara ya uongozi inayofuata uweledi *(professionalism)*, maadili ya uwazi, ukweli na haki ilisimama kidete kuhakikisha uhai na malengo, mafanikio, uhusiano mwema usiokuwa na masharti wa ndani na nje ya nchi unapatikana na kuimarishwa. Hivyi sasa ZLSC imekuwa kimbilio la wanyonge.

Mara kwa mara uongozi wa ZLSC kupitia mikutano ya waandishi wa habari, semina na makongamano haikuona aibu wala vibaya kunyoosha kidole kwa wale wote waliokuwa ndani na nje ya serikali pale walipotumia ubabe au nyadhifa zao vibaya kukandamiza haki hususan kwa wanyonge.

Tunashukuru sana kauli ya kutupa moyo na changamoto aliyoitoa Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania, Mheshimiwa Barnabas Samatta alipokuwa akitoa hotuba makhsusi *(keynote address)* katika kilele cha sherehe za miaka 20 ya ZLSC katika ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund (ZSSF), Tibirinzi, Pemba na hapa tunamnukuu kwamba:

“Kituo chenu kiendelee kujizatiti kuwatumikia Wazanzibari kwa weledi, ujasiri na upendo kama ambavyo mmefanya hadi sasa kwa miaka ishirini. Wanyonge wawezeshwe kuendelea kukiona Kituo kama ngome yao dhidi ya ubabe, uonevu au ukandamizaji utokao kwa viongozi wa Serikali au kutoka kwa watu binafsi. Lakini hapo hapo msisite kuwakumbusha wananchi kuwa hakuna haki ya kukataa kutii sheria. Demokrasia na uhuru hustawi penye nidhamu na utii wa sheria. Ulipizaji kisasi si utamaduni unaoendana na ustaarabu.”

Bodi ya Wadhamini ya ZLSC kwa niaba ya watendaji wote inatoa ahadi kwamba inachukua kauli ya Jaji Samatta kwa uzito mkubwa na inaahidi kwamba daima milele ZLSC itasimamia haki na wala haitawaangusha wazanzibari.

Tunawaombeni wote mtupe mashirikiano makubwa katika safari yetu ya kutetea haki na kufanya kazi kwa kufuata misingi ya Katiba, Sheria na Utawala Bora.

**Prof. Chris Maina Peter**
**Mhariri**

# Toeni Maoni ya Katiba Bila ya Woga - Mwanasheria Mkuu



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Othmana Masoud Othman, akitoa hotuba katika maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani, tarehe 10 Disemba 2012 katika ukumbi wa Mkutano wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar.*

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman amesema watu wapo huru kutoa maoni kuhusu Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya woga na wanaweza kutofautiana mawazo.

"Sio lazima watu wakubaliane katika kutoa mawazo kuhusu Katiba mpya. Kila mtu ana mawazo yake," alisema Mwanasheria Mkuu alipokuwa akifungua sherehe za kuadhimisha Siku ya Haki za Binadamu Duniani katika ukumbi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), Migombani.

Siku ya Haki za Binadamu Duniani inaadhimishwa Disemba 10 kila mwaka kwa utaratibu tofauti. Baadhi ya nchi hufanya maandamano, semina na makongamano ili kuadhimisha siku hii. Ujumbe wa mwaka huu ni "Sauti Yako ni Muhimu".

Mwanasheria Mkuu alisema katika zoezi la kutoa maoni kuhusu Katiba mpya watu watoe maoni yao bila ya kujali kama maoni yanafanana na maoni waliyotoa watu wengine.

"Watu wapo huru kutofautiana mawazo katika kutoa maoni kuhusu Katiba mpya," alisisitiza.

Aliipongeza ZLSC kwa juhudi ya kusaidia utetezi wa haki za binadamu na kutoa elimu ya sheria Zanzibar.

Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu yalifuatiwa na mada mbili kuhusu haki za binadamu zilizotolewa na Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania Bwana Zahor Khamis na mwanaharakati wa haki za binadamu Bwana Ally Saleh.

Kamishna Zahor aliwasilisha mada kuhusu Haki za Binadamu Zanzibar na Bwana Ally Saleh aliwasilisha mada kuhusu Rushwa.

Mwenyekiti ZLSC Profesa Chris Maina Peter alikuwa mwenyekiti katika mjadala wa mada hizo mbili.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na baadhi ya wawakilishi kutoka asasi za kiraia, dini na vyama vya kisiasa

# ZLSC Yatimiza Miaka 20

Inatoka Uk. 1

Sherehe za kutimiza miaka 20 ya ZLSC zilifanyika sambamba na kumbukizi ya maisha ya mmoja ya mwanzilishi wake marehemu Profesa Haroub ambaye alitoa mchango mkubwa wa kusaidia wanyonge kupata haki.

Kongamano la wasaidizi wa sheria lilidhaminiwa na *Open Society Initiative for East Africa* (OSIEA). Baadhi ya wataalamu wa huduma za wasaidizi wa sheria kutoka Nairobi, Kenya, Dar es Salaam, Bagamoyo na Morogoro walihudhuria.

Vile vile, wawakilishi wa asasi za kiraia, Serikali, wanasheria na wawakilishi wa Mahkama waliopo Pemba walihudhuria sherehe zilizofanyika katika ukumbi wa *Zanzibar Social Security Fund* (ZSSF) uliopo Tibirinzi, Chake Chake, Pemba.

Baadhi ya malengo ya kuanzishwa ZLSC ni kuwasaidia watu wasiojiweza kutetea haki zao kupitia Mahkama badala ya kulalamika mitaani.

Aidha, ZLSC inatoa elimu ya sheria kupitia redio, televisheni na jarida linalochapishwa kila baada ya miezi mitatu.

# Jaji Mkuu Mstaafu



*Jaji Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Barnabas Samatta*

Inatoka Uk. 1

kupeleka viwimbi vya matumaini ili kubomoa kuta za uonevu.

Jaji Samatta alisema katika dunia ya leo, taasisi zisizo za serikali zinachukuliwa kama mhimili wa tano wa dola na zikipewa uhuru zinazostahili nafasi hizo zinaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuongeza uhuru wa mwananchi na kuboresha maisha yake kwa jumla.

Alitoa changamoto kwa ZLSC iendelee kujidhatiti kuwatumikia wazanzibari kwa uweledi, ujasiri na upendo kama ilivyofanya katika miaka 20 iliyopita.

Alisema wanyonge wawezeshwe kuiona ZLSC kama ngome yao dhidi ya ubabe, uonevu na ukandamizaji utokao kwa viongozi wa Serikali au kutoka kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Jaji Samatta aliitaka ZLSC kuwakumbusha wananchi kuwa hakuna haki ya kukataa kutii sheria. Alisema demokrasia na uhuru hustawi penye nidhamu na utii wa sheria na ulipizaji kisasi si utamaduni unaoendana na ustaarabu.

Alisema vyombo vya Serikali viwajibike kwa sheria kama ilivyo kwa mwananchi na vikipinda au kuidharau sheria tiba si vurugu bali kuziomba Mahakama zitamke juu ya uhalali wa vitendo hivyo na kuchukua hatua nyengine chini ya sheria.

Aidha, alisema vyombo vya kutunga sheria vinatakiwa kuwa midomo mikuu ya wanyonge lakini mara nyengine vyombo hivyo vinakuwa vibogoyo.

Alisema asasi zisizo za Serikali zinazoshughulikia haki za binadamu na za msingi zinawajibika kujituma zaidi zikisaidiana na vyombo vyengine ndani ya nchi.

# Msaidizi wa Sheria Afariki Pemba



*Marehemu Maalim Urua Suleiman Omar*

**MSAIDIZI** wa Sheria wa jimbo la Kiwani, Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba, Maalim Urua Suleiman Omar (37) amefariki dunia Disemba 01, 2012 baada ya kupata ajali ya barabarani.

Maalim Urua alizikwa kijijini kwao, Kiwani, Disemba 02, 2012. ameacha mke na watoto watano; wanaume wanne na mwanamke mmoja.

Taarifa za Polisi kutoka Mkoa wa Kusini Pemba zilithibitisha kwamba marehemu Maalim Urua aligongwa na gari (daladala) Novemba 23, 2012 katika eneo la Mtuhaliwa alipokuwa anakwenda kazini.

Marehemu Urua alilazwa katika hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani kabla ya kufariki. Marehemu Urua alikuwa mwalimu katika Skuli ya Sekondari ya Uweleni iliyopo Wilaya ya Mkoani Pemba.

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kilimteua marehemu kuwa msaidizi wa sheria *(paralegal)* wa jimbo la Kiwani, Januari 2012 baada ya kufaulu usaili.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya ZLSC, Profesa Chris Maina Peter alimuelezea marehemu Maalim Urua kwamba alikuwa mcheshi na mwenye mashirikiano ya karibu na wenzake.

Alisema kwamba marehemu Maalim Urua ameacha pengo kubwa lisilozibika mara moja. Kwa niaba ya ZLSC, alitoa salamu za pole kwa familia, ndugu na marafiki wote wa marehemu.

Profesa Peter alimwambia Waziri wa Afya Zanzibar, Mheshimiwa Juma Duni Haji kwamba kukosekana kwa Chumba cha Wagonjwa Mahtuti *(Intensive Care Unit)* kulisababisha marehemu Maalim Urua kukosa matibabu stahili.

Waziri Duni alithibitisha kwamba hospitali ya Abdalla Mzee haina chumba cha wagonjwa mahtuti lakini alisema mpango wa kujenga chumba cha wagonjwa mahtuti kupitia ufadhili kutoka nje upo.

Huyu ni msaidizi wa sheria wa pili kufariki dunia tokea ZLSC kuanzisha mradi wa wasaidizi wa sheria mwaka 2007 ili kusaidia kutoa huduma ya sheria kwa maskini na wanyonge katika majimbo yao.

Aliyekuwa msaidizi wa sheria wa jimbo la Fuoni Wilaya ya Magharibi Mkoa wa Mjini Magharibi, Bwana Mgeni Haji Nassor alifariki dunia kwa shinikizo la damu mwanzoni mwa mwaka 2012.

# Wasaidizi wa Sheria Wafanya Mitihani



*Baadhi ya Wasaidizi wa Sheria wakifanya mitihani ya mwisho wa mwaka wa kwanza wa masomo ya msingi ya Sheria Disemba 22-23, 2012, katika Ukumbi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar.*

**WASAIDIZI** wa sheria 62 wamefanya mitihani wa kumaliza mwaka wa kwanza wa masomo yanayoendeshwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).

Mratibu wa Mradi wa Wasaidizi wa Sheria wa ZLSC, Bibi Mtumwa Said Sandal alisema kati ya waliofanya mitihani 23 ni kutoka Pemba, ambao wanawake walikuwa wanane na wanaume walikuwa 15.

Alisema waliofanya mitihani kutoka Unguja walikuwa ni 39, kati ya hao wanawake walikuwa 24 na wanaume walikuwa 15.

Alisema mitihani ilifanyika Disemba 22 na 23, 2012 Unguja na Pemba.

Wasaidizi wa sheria walifanya mitihani ya masomo manne yaliyofundishwa mwaka wa kwanza. Mafunzo ya wasaidizi wa sheria ni miaka miwili.

Masomo yaliyofanyiwa mitihani ni Sheria ya Mkataba *(Law of Contract)*, Sheria ya Uhalifu na Mwenendo wa Makosa ya Jinai *(Criminal Law and Criminal Procedure)*, Mfumo wa Sheria *(Legal Method)* na Katiba *(Constitutional and Legal System in East Africa)*.

Wasaidizi wa sheria wanatarajiwa kuanza mafunzo ya mwaka wa pili Januari 2013. Hili ni kundi la pili la wasaidizi wa sheria kufundishwa masomo ya msingi ya sheria ili kuwawezesha katika kutoa huduma za sheria.

Vile vile, Mratibu wa Wasaidizi wa sheria alisema usaili wa wasaidizi wa sheria wengine utafanyika Januari 2013 ili kuongeza idadi ya wasaidizi wa sheria waliopo katika majimbo yote 50 ya uchaguzi Zanzibar.

Alisema madhumuni ya kuanzisha mafunzo ya wasaidizi wa sheria ni kuwanoa kwa ajili ya kutoa huduma za sheria bure kwa wanyonge katika majimbo yao ili kufanikisha dhana ya kupatikana haki *(access to justice)*.

# Wasaidizi wa Sheria Wahitimu Wapewa Vyeti

**JUMLA** ya wasaidizi wa sheria *(paralegals)* 54 wamepewa vyeti baada ya kuhitimu masomo ya miaka miwili yaliyokuwa chini ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).

Mratibu wa wasaidizi wa sheria Zanzibar, Bibi Mtumwa Said Sandal, alisema kwamba kati ya wahitimu 54 waliopewa vyeti 14 walikuwa wanawake na 40 walikuwa wanaume.

Alisema kwamba wasaidizi wa sheria waliohitimu 33 ni kutoka Unguja ambao tisa walikuwa wanawake na 24 walikuwa wanaume.

Vile vile, Bibi Mtumwa alisema wasaidizi wa sheria 21 kati ya 54 waliohitimu ni kutoka Pemba ambao watano walikuwa wanawake na 16 walikuwa wanaume.

Mgeni rasmi aliyewakabidhi vyeti wasaidizi wa sheria alikuwa Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta.

Mahafali yalifanyika sambamba na kongamano la wasaidizi wa sheria lililofanyika katika ukumbi wa *Zanzibar Social Security Fund* (ZSSF).




*Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta akimkabidhi mmoja wa Wasaidizi wa Sheria wahitimu Disemba 01, 2012 katika mahafali iliyofanyika sambamba na kongamano la Wasaidizi wa Sheria katika Ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund, Tibirinzi, Pemba.*

ZLSC imeanzisha utaratibu wa kuwasomesha wasaidizi wa sheria kutoka majimbo yote 50 ya uchaguzi kutoka Zanzibar na baadhi ya maafisa wa Idara Maalum (Vikosi) na jeshi la polisi vilivyo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mwaka wa mwanzo, wasaidizi wa sheria wanasoma Sheria ya Mikataba *(Law of Contract)*, Sheria ya Uhalifu na Sheria ya Mwendo wa Makosa ya Jinai *(Criminal Law and Criminal Procedure Act)*, Mifumo ya Sheria *(Legal Method)* na Katiba *(Constitutional and Legal System in East Africa)*.

Mwaka wa pili wasaidizi wa sheria wanasoma Sheria ya Madhara *(Law of Torts)*, Sheria ya Ushahidi *(Evidence Decree)*, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai *(Civil Procedure Decree)* na Sheria ya Utawala *(Administrative Law)*.

# Wasaidizi wa Sheria Wafundishwa Kuunda Jumuiya



*Baadhi ya Wasaidizi wa Sheria, wakiwa katika mafunzo ya uundaji wa Jumuiya yaliyofadhiliwa na Shirika la Legal Services Facility (LSF) na kufanyika Disemba 03-04, 2012, katika Ukumbi wa Makonyo, Wawi, Pemba.*

**WASAIDIZI** wa Sheria wamehudhuria semina ya siku mbili ya kujadili mbinu za kuunda mtandao *(Zanzibar Paralegals Network)* kuendeleza kazi zao watakapomaliza mafunzo ya miaka miwili ya elimu ya msingi ya sheria.

Mafunzo hayo yalifanyika katika ukumbi wa Makonyo, Wawi, na kuandaliwa kwa mashirikiano baina ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) na Shirika la *Legal Service Facility* ( LSF).

Mada tano ziliwasilishwa katika mafunzo. Mada hizo ni "Mradi Mpya wa Wasaidizi wa Sheria Zanzibar," Mbinu za Kuongoza Jumuiya na Kuweza Kufanikiwa," na "Mtandao Unaohitajika Zanzibar na Mamlaka yake na kazi zake",

Mada nyengine zilikuwa ni "Mambo ya Kushirikiana Baina ya Wasaidizi wa Sheria na Wadau Wengine" na "Kupashana Habari kwa Wasaidizi wa Sheria"

# HOTUBA ILIYOTOLEWA NA MHE. JAJI MKUU MSTAAFU BARNABAS A. SAMATTA WAKATI AKIFUNGUA KONGAMANO LA KITUO CHA HUDUMA ZA SHERIA ZANZIBAR, TAREHE 30 NOVEMBA, 2012, KISIWANI PEMBA

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Profesa Chris Maina Peter;
Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba;
Waheshimiwa Viongozi mbalimbali;
Waheshimiwa Wajumbe wa Bodi;
Mheshimiwa Mrajis wa Mahakama Kuu;
Mheshimiwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo;
Waheshimiwa Mahakimu;
Wasaidizi wa Sheria;
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, napenda kukushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunialika kuwa Mgeni makhsusu kwenye ufunguzi wa Kongamano la Kituo chenu. Siku zote natambua fika umuhimu mkubwa sana wa taasisi zisizo za serikali katika maendeleo ya jamii. Hivyo, sikusita hata kidogo kuukubali mwaliko huo. Kwangu mwaliko huo ni heshima kubwa.

Kama tulivyojulishwa, Kituo kimetimiza umri wa miaka ishirini. Napenda, Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa hii kukipongeza sana Kituo kwa mafanikio hayo na mengine. Waanzilishi wa Taasisi hii, akiwemo Profesa Haroub Othman, ambaye kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu amekwisha tangulia mbele ya haki, wanastahili pongezi sana. Jamii ya Zanzibar na nje ya Visiwa hivi ina deni kubwa sana kwao.

Mafanikio ya Kituo ni mengi sana. Nitayataja machache yake:

(1) kutolewa huduma mbalimbali kwa wananchi hasa wanyonge;

(2) kutoa machapisho mbalimbali ya hali ya juu, yakiwemo yafuatayo:

  (a). Kanuni za Maadili kwa Majaji na Mahakimu wafanyao kazi Unguja na hapa Pemba;

  (b). Ripoti Juu ya Haki za Binadamu hapa Tanzania kwa miaka 2006, 2007, 2008, 2009 na 2010;

  (c). Zanzibar, Maendeleo ya Katiba; na

(3) Kuendesha mafunzo kwa Wasaidizi wa Sheria. Haya ni mafanikio makubwa sana. Mmejishughulisha na utetezi wa haki za binadamu hapa Visiwani kwa kiwango ambacho kimewavutia watu wengi sana. Mmepeleka viwimbi vya matumaini ili kubomoa kuta za uonevu. Ili kuwapa moyo napenda kunukuu maneno haya ya hekima kubwa sana ya Robert Kennedy, aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Amerika:



*Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta akitoa hotuba makhsusi katika kongamano la Wasaidizi wa Sheria lililofanyika Novemba 30,2012katika Ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund (ZSSF), Tibirizi, Chake chake Pemba.*

**"Kila wakati mtu akisimama kupigania kanuni ya maisha yasiyo na kasoro au vitendo vya kuboresha maisha ya wengine, au akipinga uonevu, anapeleka kiwimbi cha tumaini, na vikipishana kutoka vituo mbalimbali vya nguvu na ujasiri, viwimbi hivyo vinatengeneza mkondo ambao unaweza kuangusha kuta imara za uonevu na upinzani."**

Bwana Kennedy alitamka maneno haya ya kutia nguvu sana ndani ya Afrika Kusini wakati ubaguzi wa rangi nchini humo ulikuwa umepamba moto. Bila shaka maneno haya yaliwatikisa wabaguzi katika nchi hiyo.

Kwa maoni yangu – na nalisema hili kwa heshima kubwa – Profesa Othman na waanzilishi wenzake walifanya uamuzi mmoja, wakati wanaanzisha Kituo, ambao ni wa hekima kubwa sana - kujizuia kukiita hicho Kituo "Kituo cha Misaada ya Sheria". Mimi, Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kuwa matumizi ya maneno *legal aid* (msaada wa sheria) yamepitwa na wakati. Haki ya kuwakilishwa au kutetewa na mwanasheria au msaidizi wa sheria kwenye kesi au masuala mengine ya kisheria ambayo ni mazito inastahili kutambuliwa na sheria. Mfumo wa utoaji haki Mahakamani tuliorithi kutoka wa Wakoloni wa Kiingereza ulibuniwa huko Uingereza na wanasheria kutumiwa na wao. Mfumo huu umejaa kanuni na taratibu za kiufundi

sana. Hata baadhi ya mahakimu wetu wakati mwingine hutatanishwa na baadhi ya Kanuni hizo. Mfumo huo ulichukua nafasi ya mifumo ya kiafrika iliyokuwa rahisi kueleweka kwa wananchi wa kawaida. Huko Uingereza mfumo wa misaada ya sheria kwa watu maskini ulianza, kama baadhi yenu Wageni Waalikwa mnavyofahamu, miaka kama mia nane iliyopita. Mwaka 1949 mfumo huo ulifanyiwa marekebisho makubwa sana. Mmoja wa waliokuwa majaji mashuhuri sana katika nchi hiyo, Lord Denning, anauelezea mfumo mpya kwa maneno haya:

"Sheria ya kwanza ya Bunge ya Msaada wa Sheria ilipitishwa tarehe 30 Julai, 1949. Mtu sasa habanwi kuleta 'madai yake mahakamani … kwa gharama zake'.Wale ambao ni fukara – wenye uwezo mdogo – wanaweza kufungua kesi zao kwa kugharamiwa na dola. Wanaweza wakazifanya hizo kesi ziendeshwe na wanasheria wa uchaguzi wao – bila kuchangia chochote kutoka mifuko yao. Wanatoa mchango 'sufuri', kama unavyoitwa. Wakishinda kesi wanajichukulia matunda ya ushindi huo.Wakishindwa, hawawajibiki kulipa gharama za kuendesha kesi za upande mwingine. Hivyo hivyo kwa wale ambao wana uwezo zaidi kidogo wa fedha – ila kwa tofauti hii. Wanahitajika kutoa mchango mdogo – wa aina ambao wanaweza kumudu bila kujitwisha ugumu – kwa gharama za mwanasheria *(Solicitor)* wao. Kwa vyovyote kama hatua ya haraka sana inahitajika, cheti cha dharura kinaweza kutolewa: bila uchunguzi wowote kuhusu uwezo. Kinachohitajika ni mutahsari wa mwanasheria. Lakini wale walio katika hali nzuri – wa makundi ya kati ya jamii – hakuna msaada wa sheria hata kidogo. Bado wanahitajika kulipa gharama zao – na zile za upande mwingine kama wakishindwa".

Kwa maelezo haya na katika nyanja hii Waingereza wakilinganishwa na sisi Watanzania, wao ni "wajamaa" zaidi. Japo Sheria yao inatumia maneno *"legal aid"* mfumo wenyewe ni kama unaanzisha haki ya huduma ya sheria kwa wanyonge. Msaada unaweza kutolewa au kunyimwa. Mimi si mchumi. Inawezekana uchumi wetu kwa sasa hauwezi kubeba mfumo unaofanana na huo wa Uingereza. Lakini tunaweza kuanza kuelekea huko kwa kuanza kutoa haki ya huduma ya sheria kwa zile kesi nzito sana katika nyanja ya madai. Maskini mwenye nusu ekari tu hapa duniani anayoweza kuichukulia kama ardhi yake apewe huduma ya sheria kuilinda hatua hiyo inapohitajika kuchukuliwa dhidi ya wababe. Utambuzi wa kiwango fulani wa haki ya matibabu na huduma ya sheria kwa wanyonge utaendana na baadhi ya malengo makuu yaliyoorodheshwa katika Katiba zetu. Tuanze kuachana na dhana ya msaada na tukumbatie dhana ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sote tulio kwenye Ukumbi huu tujuavyo, dunia ya leo inatawaliwa na dhana za demokrasia na utawala wa sheria. Lakini demokrasia si dhana iliyoganda; inakua na inapanuka kadri jamii inavyopiga hatua za maendeleo katika nyanja mbalimbali, hasa zile za uchumi, elimu na jamii. Tuchukue mifano miwili: intaneti, mtandao wa mawasiliano ya kimataifa wa kikompyuta, imepanua sana mipaka ya uhuru wa maoni na kueleza fikra zake mwananchi. Hata watu walio Damascus kule Syria na Goma kule Congo wana uwezo mkubwa zaidi wa kujua yanayotokea katika miji yao kuliko ilivyokuwa



*Baadhi ya washiriki wakiwa katika Ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund, Tibirinzi, Chake chake Pemba wakimsikiliza Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta akitoa hotuba makhsusi katika kongamano la Wasaidizi wa Sheria lililofanyika Novemba 30, 2012, kuanzia kulia ni Bi. Jina Mwinyi Waziri (Afisa Mipango), Bi. Salma Haji Saadat (Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini), Bi. Frieda Pereira (Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini), Bi. Jedidah Wakonyo Waruhiu (Legal Resources Foundation-Nairobi), na Bw. Charles Nyukuri (Legal Resources Foundation-Nairobi)*



*Baadhi ya walioshiriki katika kongamano la Wasaidizi wa Sheria wakiwa katika picha ya pamoja na Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta mstari wa mbele wa pili kutoka kulia. Kushoto kwake ni Mhe. Amrani Afisa Mdhamini Afisi ya Makamu wa pili wa Rais muda mfupi baada ya Jaji Samatta kutoa hotuba makhsusi.*

miaka ya huko nyuma. Madikteta duniani wanasumbuliwa sana na mfumo wa intaneti. Mfano wa pili unahusu haki ya maandamano. Sasa haki hii inatingisha nchi nje ya Bara la Ulaya na Amerika. Japo kwa shida, na kwa wakati mwingine kwa hofu kubwa, watu wanaandamana kudai yale wanayoyachukulia kama haki zao kule Asia, Amerika ya Kusini na hapa Afrika. Bahati mbaya katika baadhi ya nchi katika mabara hayo polisi bado wana mitazamo ya mfumo wa chama kimoja. Wanakataza maandamano hata pale ambapo ni wazi kabisa kuwa hakuna hatari yoyote ya usumbufu mkubwa au amani kuvurugwa. Wanaweka pazia la chuma kutenganisha watawala na watawaliwa. Kwa nini watawala wasifahamu kutoka kwa wale wenyewe waliowaweka madarakani wanachotaka au wasichotaka kutoka kwao? Kwa nini, kwa kutumia maandamano, baadhi ya watawaliwa wasiwajulishe wananchi wenzao yale yanayowakera ili wawasaidie katika madai yao hayo? Inavyoonekana, baadhi ya maafisa wa polisi wanayachukulia maandamano kama fadhila na si kama haki. Mtazamo huo ni potofu na ni hatari. Yanayowasumbua wananchi yakilazimishwa yabaki mioyoni mwao hilo si kwa faida ya watawala. Ningependa wale maafisa wa Jeshi letu la Polisi, ambao wanaminya uhuru wa kuandamana wa wananchi wakumbuke ujumbe mzito uliomo kwenye maneno yafuatayo yaliyotamkwa na moja ya mahakama zinazoheshimiwa sana duniani, Supreme Court ya India:

**"… katika demokrasia siyo lazima kila mtu aimbe wimbo huo huo.Uhuru wa mawazo ni wa msingi sana na kwa jumla unachukuliwa kama kitu cha kawaida. Kila mtu ana haki ya msingi juu ya suala lolote linalogusa watu kwa jumla.Anaweza kuwa na maoni na kutoa habari kwa njia yoyote halali."**

Bila shaka hata haki ya kuandamana ina mipaka.Uhuru wa mtu mmoja au kikundi kimoja unaishia pale uhuru wa mtu mwingine au kikundi kingine unapoanzia. Lakini mipaka ya uhuru huo yanawekwa na sheria na siyo na polisi. Polisi ni watekelezaji tu. Ni msingi muhimu sana wa sheria katika nchi yetu kuwa mamlaka chini ya sheria iliyotungwa na chombo cha kutunga sheria hayana budi kutumiwa kwa mujibu ya malengo ya sheria yenyewe, kwa namna inavyostahili na kwa haki, na siyo kwa upendeleo, uonevu au woga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika demokrasia ya dunia ya leo, taasisi zisizo za serikali zinachukuliwa kama mhimili wa tano wa dola. Zikipewa uhuru zinazostahili, taasisi hizo zinaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuongeza uhuru wa mwananchi na kuboresha maisha yake kwa jumla.Inapoanza safari nyingine ya miaka ishirini, Kituo chenu kiendelee kujizatiti kuwatumikia Wazanzibari kwa weledi, ujasiri na upendo kama ambavyo mmefanya hadi sasa kwa miaka ishirini. Wanyonge wawezeshwe kuendelea kukiona Kituo kama ngome yao dhidi ya ubabe, uonevu au ukandamizaji utokao kwa viongozi wa Serikali au kutoka kwa watu binafsi. Lakini hapo hapo msisite kuwakumbusha wananchi kuwa hakuna haki ya kukataa kutii sheria. Demokrasia na uhuru hustawi penye nidhamu na utii wa sheria. Ulipizaji kisasi si utamaduni unaoendana na ustaarabu. Vyombo vya Serikali vinawajibika kwa sheria, kama ilivyo kwa mwananchi. Viikipinda au kuidharau sheria tiba si vurugu, bali kuziomba mahakama zitamke juu ya uhalali wa vitendo hivyo na kuchukua hatua zingine chini ya sheria kama jibu lao ni kuwa vyombo hivyo viliondoka kwenye mkondo wa sheria.Kwa kawaida vyombo vya kutunga sheria vinatakiwa kuwa midomo mikuu ya wanyonge, lakini mara zingine vyombo hivyo vinakuwa vibogoyo.Hali hiyo inapojitokeza, asasi zisizo za Serikali zinazoshughulikia haki za binadamu na za msingi zinawajibika kujituma zaidi, zikisaidiana na vyombo vingine ndani ya nchi. Kuna mambo mengi ambayo sisi

wa Tanzania Bara tutajifunza kutoka kwenu, Mhe. Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi wowote kuwa Marehemu Haroub Othman alitoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Kituo chenu na katika nyanja zingine. Nilikuja kumfahamu marehemu katika kipindi nilichokuwa Jaji Kiongozi. Alinivutia sana na upole na mitizamo yake juu ya masuala mbalimbali yaliyohusu jamii, yakiwemo demokrasia, usawa wa binadamu mbele ya sheria na umuhimu wa kuwalinda wanyonge dhidi ya uonevu na ukandamizaji. Sikushangaa niliposikia kuwa alikuwa mmoja wa waanzilishi wa Kituo cha Huduma za Sheria hapa Visiwani. Katika kila nchi hujitokeza watu ambao huamua kutumia ujuzi, weledi na uzoefu wao katika taaluma na nyanja zingine kuwatumikia wanyonge ili wafaidi haki zao chini ya Katiba na sheria zingine na kutoa huduma hizo bila malipo yoyote kwao.

Nchi yetu haijakosa kuwa na watu wa aina hiyo. Profesa Haroub Othman alikuwa mmoja wa watu wa aina hiyo. Inafurahisha sana kuwa wapo watu hapa nchini ambao wanamuenzi kwa kuendeleza mambo mema mengi aliyopigania, aliyoanzisha na aliyokuwa anatekeleza kabla Mwenyezi Mungu hajamwita. Inanipa furaha kubwa sana kusema kuwa baadhi ya watu hao wamo ndani ya Ukumbi huu. Bahati nzuri katika tafuta yangu nimeyakumbuka maneno yaliyoandikwa na Robert Louis Stevenson, mwandishi, mshairi na mwandishi wa insha wa huko Scotland aliyeishi zaidi ya miaka mia moja iliyopita, wakati alipozungumzia vigezo vya kumpima mtu aliyeondoka duniani kama alikuwa mtu mwema. Napenda kuwahakikishia Bibi Othman na familia kuwa sina hata kivuli cha shaka kuwa maneno hayo yanastahili kutumika kwa mpendwa wao, Marehemu Profesa Othman. Kwa heshima kubwa nayanukuu maneno hayo:

**"Mtu atakuwa amefanikiwa aliyeishi vyema; amecheka mara nyingi na amewapenda wengine; ambaye ameweza kupata heshima kutoka kwa watu wenye akili …; ambaye ametimiza wajibu wake; ambaye ameiacha dunia mahali pazuri zaidi kuliko alivyoikuta; … ambaye alitafuta kutoka kwa wengine uwezo wao mkubwa na aliyetumia uwezo wake mzuri kikamilifu."**

Mwenyezi Mungu, mwenye uwezo usio na mipaka, aiweke roho ya Marehemu Profesa Haroub Othman mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti; Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa; Waheshimiwa Wajumbe wa Bodi; Mheshimiwa Mkurugenzi Mtendaji; Waheshimiwa Wageni Waalikwa; Wasaidizi wa Sheria; Mabibi na Mabwana, ninashukuru kupewa nafasi hii ya kutoa hotuba *(keynote address)*. Nawatakia majadiliano ya manufaa makubwa kwa nchi yetu na Kituo chenyewe.

**Nawashukuru sana kwa kunisikiliza.**



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya ZLSC Profesa Chris Maina Peter akimkabidhi zawadi Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta baada ya kumalizika kwa kongamano la Wasaidizi wa Sheria, katika Ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund (ZSSF), Tibirinzi, Chake Chake Pemba, Disemba 1, 2012.*



*Jaji Mkuu Mstaafu wa Tanzania Mheshimiwa Barnabas Samatta akichambua Karafuu Pemba. Jaji Samatta alikuwepo Pemba kushiriki kongamano la Wasaidizi wa Sheria lililotayarishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) Novemba 30, 2012.*



*Baadhi ya Wasaidizi wa Sheria wakifanya mitihani ya mwisho wa mwaka wa kwanza wa masomo ya msingi ya Sheria Disemba 22-23, 2012, katika Ukumbi wa Kituo cha Huduma za Sheria Chake Chake Pemba, Zanzibar.*




*Walioshiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu wakiwa katika picha ya pamoja na Mgeni rasmi Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Disemba 10,2012 nje ya Ukumbi wa Mikutano wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).*



*Wafanyakazi na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) wakisikiliza hotuba ya Mwenyekiti Profesa Chris Maina Peter katika tathmini (retreat) ya utendaji kazi mwaka 2012, iliyofanyika katika Ukumbi wa Visitors' Inn, Jambiani,Unguja.*




*Wadau wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) katika picha ya pamoja baada ya kumaliza kikao chao kilichofanyika Disemba 9, 2012, katika ukumbi wa ZLSC, Migombani, Zanzibar.*



*Baadhi ya Maafisa Mipango wa ZLSC, Pemba, wakitoa msaada wa sheria katika Siku ya Msaada wa Kisheria Duniani Disemba 13, 2012 katika Skuli ya Micheweni Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.*

# Hatua ya Awali ya Uendeshaji Kesi ya Jinai

Na Safia Saleh, ZLSC, Pemba



*Mezani ya Haki.*

**Utangulizi**

Uendeshaji wa kesi ya jinai katika Mahkama umegawika katika sehemu mbali mbali. Kwa mfano hatua ya kwanza ni kusomwa shtaka na kupewa nafasi mshtakiwa kukiri au kukataa kosa, kuahirishwa kesi ili kutoa nafasi upande wa mashtaka kutayarisha ushahidi, kusikilizwa pingamizi za awali kama zipo, kesi kusikilizwa, upande wa mshtakiwa kupewa nafasi ya kutoa maelezo yake na kumhoji au kuwahoji mashahidi, kufunga uwasilishaji wa maelezo na hatimaye Mahkama kutoa hukumu ya kesi husika. Makala hii itaelezea namna kesi ya jinai inavyoendeshwa na wajibu wa mshtakiwa.

**Maana ya kosa la jinai**

Kosa la jinai ni kosa au makosa yaliyoorodheshwa katika Sheria za Jinai katika nchi husika. Inawezekana kitendo kikawa kosa katika nchi moja na kisiwe kosa katika nchi nyengine. Kwa mfano, Zanzibar inatumia Kanuni za Adhabu *(Penal Act No. 6 ya 2004),* Sheria za Zanzibar. Kosa au makosa ya jinai yanapofanywa, anayeshtaki ni utawala *(Crown)* na aliyetendewa kosa anakuwa shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka. Mahkama inasikiliza pande zote mbili na ikiridhika na ushahidi uliotolewa mbele ya Mahkama, hukumu inatolewa.

**Maana ya mshtakiwa**

Mshtakiwa ni mtu anayeshtakiwa kutenda kosa la jinai. Serikali ndio inayoshtaki. Mshtakiwa hatochukuliwa ametenda kosa mpaka Mahkama itakapomtia hatiani bila ya kuacha shaka yoyote kwamba mshtakiwa ametenda kosa analoshtakiwa.

**Uendeshaji wa shtaka la jinai**

Siku ya kwanza ya kesi mbele ya Mahkama, mshtakiwa lazima asomewe shtaka au mashtaka anayokabiliwa nayo. Upande wa mashtaka huwasilisha shtaka au mashtaka kwa njia ya hati ya mashtaka. Ni lazima mshitakiwa awepo Mahakamani kujibu shitaka; ama kukubali au kukataa. Shtaka dhidi ya mshtakiwa linaweza kusomwa katika Mahkama hata ikiwa mshtakiwa hayupo.

Shtaka litasomwa katika Mahkama na Hakimu au Karani wa Mahkama. Kifungu cha 212 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Namba 7 ya 2004), Sheria za Zanzibar, kinasema "mahkama ni lazima imsomee mshtakiwa shtaka analokabiliwa nalo na imuulize kama anakubali au anakataa" (tafsiri isio rasmi)

Maelezo ya shtaka na muhtasari wake lazima kusomwa mbele ya mshtakiwa.

**Wajibu wa mshtakiwa**

Mambo manne hutokezea shtaka au mashtaka yanaposomwa.

1. Kukubali kosa;
2. Kukana kosa;
3. Kutoa pingamizi za awali;
4. Kunyamaza kimya.

**Kukubali kosa**

Ikiwa mshtakiwa atakubali kosa Mahkama itajiridhisha kuwa mshtakiwa amekubali kosa kwa kurikodi namna mshtakiwa alivyokiri kosa hilo. (Kifungu cha 212(2) Sheria hii kinaeleza "ikiwa mshtakiwa atakiri kosa analokabiliwa nalo basi Mahkama itarikodi kukubali kwake huko………" (tafsiri isio rasmi).

Ni wajibu wa Mahkama kuutaka upande wa Mashtaka kuthibitisha kosa ijapokuwa mshtakiwa ameungama au la. Kwa mfano kosa la "wizi" mshtakiwa akasema "ndiyo nilichukua vitu vilivyotajwa", majibu haya hayatoshelezi kuthibitisha kuwa mshtakiwa anaungama shtaka la wizi maana kuchukua mali ya mwengine tu sio wizi mpaka mali hio iwe imechukuliwa bila ya idhini ya mwenyewe.

Katika kesi ya ***Musa Muya v. Republic*** [1962] E.A 643

Mshtakiwa katika kesi hii alikabiliwa na shtaka la kusafirisha mahindi bila ya kibali. Majibu ya shtaka yalikuwa "naelewa shtaka, nakubali sikuwa na kibali lakini nilikuwa napeleka mahindi hayo Tala ilikuwa makosa"

Hakimu alimtia hatiani mshtakiwa kwa ikirari yake. Rufani ya mshtakiwa ilidhihirisha kuwa hakuungama shtaka. Tala lilikuwa ni soko ambalo mshtakiwa alisema anapeleka mahindi yale, soko hilo lilikuwa katika wilaya ile ile aliyokuwa anaishi mshtakiwa na sheria haikukataza kusafirisha mahindi ndani ya wilaya moja.

Ikiwa mshtakiwa atakiri kosa kauli yake ya kukiri kosa itarikodiwa. Waendesha Mashtaka wanaonywa kwamba mshtakiwa kukiri kosa, upande wa mashtaka lazima uthibitishe vipengele

# Hatua ya Awali ya Uendeshaji Kesi ya Jinai

vyote vya kosa na kutoa maelezo ya kina kuhusiana na maelezo hayo.

Katika kesi ya ***Yonasi Eegalu and Others v. Republic*** (9 EACA) 65 inaeleza kwamba mshtakiwa anayekiri kosa lazima akiri kila kipengele.

**Kukana kosa**

Iwapo Mshtakiwa atakana kosa, Mahkama inaweza kuamua kusikiliza au kuahirisha na kupanga tarehe ya kuanza kusikiliza na kuutaka upande wa mashtaka kuwasilisha ushahidi wake pamoja na kuwaleta mashahidi Mahkamani. Kifungu cha 213, Sheria hii (ikiwa mshtakiwa atakana kosa aliloshtakiwa nalo, Mahkama itaendelea kulisikiliza shauri hilo kwa kuwaita mashahidi kutoa ushahidi wao (tafsiri isio rasmi)

Hata hivyo, kabla ya kuahirisha kesi Mahkama itaamueleza mshtakiwa haki yake ya kupata dhamana ikiwa kesi siyo miongoni mwa kesi ambazo dhamana haitolewi kisheria

**Kunyamaza kimya**

Mshtakiwa anaweza kukataa, kukubali kosa au akanyamaza kimya au asijibu moja kwa moja kuhusu shtaka. Ikiwa Mahkama itajiridhisha kwamba mshtakiwa amefahamu shtaka alilosomewa, itachukuliwa kwamba mshtakiwa amekataa kosa.

Katika shauri la ***Wachira s/o Murage nd Others v. Republic.*** (1956) 23 E.A.C.A. 562) mshitakiwa, ambaye alikuwa amekabiliwa na shitaka la mauaji ya kukusudia, alikataa kujibu shitaka la mauaji. Jaji aliandika kuwa mshitakiwa huyo amekana shitaka. Lakini mshitakiwa aliendelea kufanya fujo wakati wa kusikiliza shauri hilo ikawa vigumu kuzikilizana. Jaji aliamuru apelekwe kwa daktari wa maradhi ya akili na imegundulikana kwamba alikuwa ni mtu mwenye akili timamu.

**Pingamizi za awali**

Zipo pingamizi za awali kadhaa zinazoweza kuelezwa Mahkamani. Kwa mfano, mshtakiwa ametoa hoja ya kwamba aliwahi kushtakiwa Mahakamani kwa kosa ambalo anakabiliwa nalo sasa na hukumu ilitolewa au amepata msamaha wa Rais kwa kosa kama hilo.

Ili pingamizi ya aina hiyo ikubaliwe, Mahkama itajiridhisha yafuatayo;

(a) Mshtakiwa aliwahi kushtakiwa kwa kosa kama hilo na sasa anashtakiwa tena kosa hilo.
(b) Maelezo ni sawa na kosa la awali.

Katika ***Republic v. Absolon Muhanga na Mwenzake*** (1957) E.A. 660, washtakiwa walishtakiwa kosa la kubaka. Washtakiwa walitoa hoja kuwa tayari walishtakiwa na kutiwa hatiani kutokana na kosa la kuvuruga amani na nidhamu katika Jeshi la Polisi. Maelezo ya shtaka lile la awali na la sasa yalikuwa sawa.

Hakimu aliyesikiliza shitaka hilo kwa mara ya mwanzo alikubali majibu ya washitakiwa. Jamhuri ilikata rufaa dhidi ya uamuzi huo na Mahakama Kuu ilisema kwamba ili hoja kama hiyo ikubaliwe, kosa la awali ni lazima liwe sawa na lile la sasa au hata kama sio sawa kabisa basi likaribiane sana.

Dhana inayojadiliwa hapa kwamba mshtakiwa haadhibiwi mara mbili kwa kosa moja.

**Changamoto**

1. Baadhi ya wakati waendesha mashtaka husoma muhtasari tu wa mashtaka kuhusiana na kosa bila ya kueleza undani wa mazingira ya shtaka husika.
2. Mara nyingi washtakiwa huungama shtaka kwa sababu ya kutoelewa vipengele vya kosa.

**Mapendekezo**

1. Mwendesha Mashtaka atoe maelezo ya kutosha ya shtaka kumuwezesha mshtakiwa afahamu shtaka na kutoa majibu yake vizuri.

2. Maelezo ya shtaka kusomwa vizuri ili kumpa nafasi mshtakiwa kutafakari majibu na kutoa nafasi kwa hakimu au jaji kurikodi vyema.

**Hitimisho**

Hati ya mashtaka ni dira na msingi katika kesi ya jinai. Hati ya mashtaka hueleza kosa na muhtasari wa kosa. Hati ya mashtaka inatoa mwanga upande wa utetezi kujiandaa dhidi ya kosa.



*Jengo la Mahakama ya Chake Chake Pemba*

# Utoaji Leseni Holela Kumeongeza Ajali Barabarani

Na Moh'd Hassan, ZLSC, Pemba




*Ajali za barabarani zinavyoathiri mali na usalama wa raia baadhi yake husababishwa na madereva wasiokuwa na sifa za kuendesha vyombo vya barabarani.*

## Utangulizi

ONGEZEKO la ajali za barabarani ni matokeo ya kutoelewa au kudharau kuheshimu sheria au rushwa kwa baadhi ya watendaji na kusababisha sheria kutotekelezwa. Ajali husababisha athari kadhaa; kwa mfano haki ya kuishi inakatizwa, mali na miundo mbinu ya barabara kuharibika. Taasisi husika za utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Barabarani Nam. 7 ya 2003 ikiwemo jeshi la polisi, Idara ya Ukaguzi na Vyombo vya Barabarani na Utoaji Leseni na Mahkama zinanyoshewa kidole kushindwa kutekeleza wajibu wao. Makala hii inazungumzia utaratibu wa utoaji leseni za vyombo vya barabarani.

Sheria ya Usafiri wa Barabarani Nam. 7 ya 2003 imegawika sehemu kadhaa ikiwemo utaratibu wa utoaji leseni za barabarani. Zipo aina mbali mbali za utoaji wa leseni na vigezo vinavyotumika kutoa leseni hizo.

## Maana ya leseni

Leseni ni kibali kinachotolewa na taasisi iliyopewa mamlaka kisheria kumruhusu mtu kuendesha chombo cha moto.

## Aina za leseni

Katika utaratibu wa kutoa leseni za udereva, vyombo vimegaiwa katika daraja zifuatazo kwa mujibu wa Kifungu cha 82(1) cha Sheria hii.

A - Vyombo vya maringi mawili

BI - Vyombo vya watu binafsi vinavyochukua hadi watu saba

B - Vyombo vya binafsi vinavyochukua zaidi ya watu saba

CI - Gari za mizigo zinazobeba uzito usiozidi kilo 3,500

C - Gari ya mizigo zinayobeba uzito unaozidi kilo 3500

D1 - Gari za umma zilizo na viti saba

D - Gari za umma zilizo na viti zaidi ya saba

E - Trekta

G - Aina zote za vyombo vya moto

M - Mopedi

Waziri husika katika Wizara inayohusiana na leseni amepewa madaraka kwa kushauriana na mamlaka husika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la serikali anaweza kubadilisha au kuengeza daraja la gari

## Taasisi inayotoa leseni

Taasisi yenye mamlaka ya usafiri barabarani ina dhamana ya kutoa leseni au kukataa kutoa leseni ya

# Utoaji Leseni Holela Kumeongeza Ajali Barabarani

udereva, leseni ya mwalimu wa udereva ,kusimamisha leseni ya dereva itakapoona inafaa kufanya hivyo

**Sifa za muomba leseni**

Leseni ya udereva inatolewa kwa mtu mwenye sifa zifuatazo:-

a) miaka 16 - daraja M
b) miaka 18 - daraja A, BI na CI
c) miaka 21 - daraja B, C, DI. E
d) miaka 25 - daraja D
e) miaka 25 - daraja G

**Muda wa leseni**

Iwapo haikusalimishwa au kukatishwa, leseni itadumu na kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja hadi miaka mitatu kuanzia tarehe iliyotolewa.

**Kufutwa leseni**

Mahakama inaweza kuamrisha kufutwa leseni au kuizuia leseni kwa kipindi maalum. Mtu anaweza kunyimwa leseni ikiwa atakuwa chini ya umri, kuwa na leseni zaidi ya moja au kupoteza sifa ya kuwa na leseni.

**Dereva kuwa na leseni anapoendesha chombo**

Mtu hataruhusiwa kuendesha chombo bila ya kuwa na leseni halali. Ni wajibu wa dereva kuwa na leseni wakati wote anapoendesha chombo na kuitoa leseni pale inapohitajika na askari barabarani.

Endapo dereva atashindwa kuonyesha leseni au kuiwasilisha kituo cha polisi au sehemu yoyote aliyoambiwa ndani ya saa 24 atakuwa na hatia atalipa faini au kifungo kisichopungua mwezi mmoja.
Si ruhusa mmiliki au mdhamini wa gari kumruhusu mtu asiekuwa na leseni kuendesha gari.

**Leseni za Kimataifa kutambulika na kutumika Zanzibar**

Zanzibar inatambua leseni iliyosajiliwa Kimataifa au nje ya nchi isipokuwa kwa mazingira maalum, mtu mwenye leseni ya aina hiyo atatakiwa kuiwasilisha katika mamlaka husika kwa kuthibitishwa na kusajiliwa.

**Changamoto za Kisheria katika utoaji wa leseni**

1. Uelewa wa sheria kwa madereva, watumiaji wa barabara na vyombo vinavyohusiana na usalama barabarani ni mdogo.

2. Rushwa inachangia utoaji wa leseni holela.

3. Askari wa barabarani hawafuati sheria ya kuwataka madereva kuwasilisha leseni katika kipindi kinachohitajika.

**Mapendekezo.**

1. Jamii kuelimishwa sheria ya usafiri barabarani.

2. Kuna haja ya sheria kupitiwa upya hususan katika viwango vya fedha za adhabu.

3. Vyombo vya Serikali vipewe leseni ya barabara.

4. Madereva wazembe wanyang'anywe leseni.

**Hitimisho**

Sheria ya Usalama Barabarani iheshimiwe ili kupunguza ajali zinazoepukika. Utaratibu wa kutoa leseni uboreshwe ili kuziba mwanya kutoa leseni holela.



*Taa za kuongozea vyombo vya barabarani pamoja na watumiaji wa barabara zilizopo Mkunazini Zanzibar ambazo zimeharibika kwa muda mrefu sasa bila ya kuonekana jitihada za kuzikarabati*

# Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani 10 Disemba 2012



*Kamishna Zahor Khamis akitoa mada kuhusu haki za Binadamu Zanzibar katika maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani Disemba 10,2012 katika Ukumbi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar.*

**Utangulizi.**

TAREHE 10 Disemba ya kila mwaka inaadhimishwa kimataifa kuwa ni Siku ya Haki za Binadamu Duniani. Kihistoria tarehe hii inaturejesha nyuma mwaka 1948 wakati ambapo Umoja wa Mataifa Ulipitisha Azimio la Haki za Binadamu *(Universal Declaration of Human Rights – 1948).*

Azimio hilo ili kulipa nguvu ya utendaji lilifuatiwa na mikataba miwili ya Kimataifa ambayo ni:-

1. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 *(International Covenant on Civil and Political Rights)*

2. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni 1966 *(International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights).*

Mikataba hii imeridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo basi, Tanzania inafungika kutekeleza mikataba hiyo na kwa kuonekana katika sheria zake na kwa matendo yake.

**MAADHIMISHO YA SIKU YA HAKI ZA BINADAMU DUNIANI 2012**

Siku ya Maadhimisho ya Haki za Binadamu kwa kila mwaka hupewa kauli mbiu ikiwa na maana ya kujitathmini, kukuza na kutetea haki za binadamu. Kauli mbiu ya kimataifa kwa mwaka huu ni *"MY VOICE COUNTS".*

Mwaka huu 2012 tunaadhimisha miaka 64 ya Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu ambapo kwa kauli mbiu ya mwaka huu "my voice counts"-"Sauti yangu inachangia" ambapo kauli mbiu hiyo inajielekeza katika Ibara za Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu la 1948 ikijumuisha na Haki za kujieleza *(Freedom of Expression),* Haki ya kushiriki katika chaguzi *(the right to participate in elections)*, Haki ya Kushiriki katika maamuzi *(the right to take part in institutional decision making)* na Haki ya uhuru wa kukutana na uhuru wa kujiunga pamoja *(the right to freedom of assembly and freedom of association)*. Kwa kauli mbiu ya mwaka huu, pamoja na kuzingatia Ibara za Azimio la Haki za Binadamu pia linakwenda sambamba na mazingatio ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

Haki za Binadamu katika mazingira ya Zanzibar.

Uwepo wa Azimio la Haki za Binadamu pamoja na ile mikataba miwili niliyoitaja hapo juu kwa kiwango kikubwa Ibara hizo zinazopatikana katika nyaraka zinazosomeka katika Katiba zetu na Sheria zetu, lakini kwa kuzingatia madhumuni ya siku hii ya leo, hatuna budi kujitathmini katika matendo na mapungufu yetu pamoja na changamoto zinazotukabili katika utii wetu na malengo ya maadhimisho ya siku hii ya leo.

Haki ya Kiuchumi inajumuisha fursa na harakati halali za kazi mbali mbali ambazo humuwezesha binadamu kupata mahitaji au kipato cha kujikimu kuendesha maisha yake. Hii inaweza kuwa kazi za kilimo, biashara

# Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani 10 Disemba 2012

na ajira mbali mbali. Ufanisi wa kazi zote hizo unategemeana na mazingira mazuri yaliyowekwa ili kujenga tija, kukuza kipato na kukusanya kodi. Hata hivyo zipo changamoto nyingi zinazowanyima wananchi haki na fursa za kufaidi haki hizo zikiwemo:-

- Kutokuwa na mfumo endelevu na unaoeleweka wa soko na hasa pale bidhaa zinapozidi mahitaji ya soko.

- Fukuzafukuza za Manispaa za mara kwa mara kwa wafanyabiashara ndogo ndogo tena bila kuwa na maelekezo sahihi wapi waende na kulingana na aina za biashara zao.

- Kwa upande wa waajiriwa yapo matumizi mabaya ya sheria za kazi ikiwa ni pamoja na tafsiri zisizo sahihi ambapo athari zake huelekea kumkandamiza mfanyakazi, chuki kazini, mahusiano mabaya kati ya Muajiri na Mfanyakazi. Mfano wa hayo ni likizo bila malipo wanazopewa wafanyakazi katika sekta binafsi. Uhalali wa kisheria ni kwamba ili likizo ziweze kuwa halali ni lazima wafanyakazi husika wawe wameajiriwa katika mikataba ya kudumu, uhalisia ni kwamba wafanyakazi wengi wameajiriwa katika masharti ya muda maalum. Kwa upande wa Sekta za Umma ni kwamba yapo matumizi mabaya ya kanuni za utumishi Serikalini, na zaidi hutumika kwa kutoa adhabu kuliko kutoa haki na fursa zilizoelezwa na kanuni hiyo.

- Migogoro ya ardhi kwa sasa ni mingi na Mahakama zinaelekea kuelemewa na kesi. Pengine ni busara kwa sasa tukafikiria njia mbadala ya usuluhishi kuliko huu utaratibu wa kuendelea na kesi mahakamani na kusubiri mshindi wa kesi kwani hata baada ya hapo chuki huendelea.

**Haki ya Elimu.**

Zanzibar imefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana kuandikisha watoto wanaostahiki kwenda shule, shule nyingi zimejengwa na zinaendelea kujengwa mjini na vijijini. Hata hivyo mazingira ya shule zetu hasa za msingi sio rafiki kwa mahitaji ya mtoto kielimu na yana mchango mkubwa katika kuvunja haki ya mtoto.

- Watoto wengi bado wanakaa chini (bila madawati) tena katika sakafu zilizojaa vumbi.
- Huduma ya maji safi na salama kwa wanafunzi mashuleni hafifu au haipo kabisa.
- Huduma za vyoo haziridhishi hata kidogo.
- Mfumo wa utoaji wa elimu wa *large class* ambapo idadi ya wanafunzi kwa darasa hufikia 70 mpaka 90 (jee ni kweli mfumo huu unatusaidia na unatupatia tija?)
- Madrasa zetu za qur-ani zinajaza watoto wengi kupita kiasi na nyingi ya madrasa hizo mfumo wa vyoo na maji safi na salama (na maji ya kunywa) sio wa uhakika.

**Haki za kisiasa.**

Kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, Zanzibar imepita katika misukosuko na mawimbi mazito. Kwa kiwango kikubwa misukosuko ya Zanzibar inatokana na mambo mengi ikiwemo mapokeo ya dhana ya demokrasia tofauti na uhalisia, kutokuvumiliana kisiasa, kutothaminiana, kutoaminiana, ubinafsi na kubwa zaidi badala ya siasa kutumikia wananchi hali imekuwa ni kinyume chake.

**Haki nyenginezo.**

Tunapozungumzia Haki za Binadamu kwa upande wa Waafrika pia tunayo mikataba yetu ya kikanda, miongoni mwa mikataba hiyo ni Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu *(The African Charter on Human and Peoples' Rights)*. Mkataba huu unazingatia haki na wajibu kwa mazingira ya kiafrika.

Katika miaka ya hivi karibuni nchi zetu za Ulimwengu wa tatu zikiwemo za kiafrika zimekumbwa na wimbi kubwa la kuburuzwa kutambua haki za makundi kama ya mashoga, biashara ya ukahaba, usagaji na ndoa za jinsia moja. Kulazimishwa huko kumeandamana na matishio ya kunyimwa kwa misaada. Uhalisi ni kwamba mazingira ya kiafrika mambo hayo hayakubaliki na kinyume na tamaduni nyingi za kiafrika. Zaidi ya hayo kwa Tanzania mambo hayo ni kinyume na sheria zetu na ni makosa ya jinai aidha yanapingana na mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

**Hitimisho**

Kwa kauli mbiu yetu ya mwaka huu sauti yangu inachangia, kila mmoja wetu ni vyema akajipima kwa kiwango gani anachangia katika kudumisha Haki za Binadamu na anapaza sauti yake kutetea haki hizo.

Jumuiya za Haki za Binadamu kama vile Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na taasisi nyengine mbali mbali hatuna budi kujitoa kwa kukemea, kukosoa na kuelekeza njia sahihi kwa kuzingatia Utawala Bora na Haki za Binadamu.



*Baadhi ya Washiriki wa Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani Disemba 10, 2012, wakisikiliza Mjadala kuhusu Haki za Binadamu Zanzibar uliotolewa na Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar Mheshimiwa Zahor Khamis.*

# Shairi

## TUUNGANE TUZIPINGE, ADHABU ZA KIKATILI

1. Jamii ina tatizo, Mashakani meingia.
Jambo hili ni kikwazo, Kwa haki kusimamia.
Hukumu zitolewazo, Bila kufata Sheria.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

2. Yamekuwa mazowea, Sheria kujitwalia.
Mtu aliyekosea, Kipigo humwelemea.
Mawe twamuangushia, hapati kujitetea.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

3. Twajitolea adhabu, kwa Sheria mikononi.
Wahalifu twaadhibu, Tuhuma za mitaani.
Ni vitendo vya aibu, Raia tuamkeni.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

4. Ni kinyume kwenye haki, Kutesa mtuhumiwa.
Utu anastahiki, Na heshima kuwekewa.
Adhabu hastahiki, Hadi ashehukumiwa.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

5. Wakosaji kuwarudi, Kwa jambo kutuhumiwa.
Adhabu za makusudi, Kwa mapanga kuwauwa.
Tungojeni ushahidi, Na kesi kuamuliwa.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

6. Mtu moto kumchoma, Kuiba katuhumiwa.
Ni adhabu za kinyama, Jamii inazotoa
Tunaondoa heshima, Na utu umepotea.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

7. Kuwapiga wahalifu, Kwa tuhuma twakosea.
Maisha twayatilifu, Wengine tunawauwa.
Twaonyesha udhaifu, Hatuheshimu Sheria.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

8. Ni thamani ya kiatu, Maisha kuyagharimu?!
Haya si katika utu, Twaacha Ubinadamu.
Haikubaliki katu, Roho zao kudhulumu.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

9. Mtendaji wa makosa, Napelekwe Sheriani.
Sheria itadodosa, Ukweli kuubaini.
Wakosaji kuwatesa, Twajitia hatiani!
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

10. Vitendo hivi si haki, Twapaswa kuvikemea.
Mkosa astahiki, Uchunguzi kufanyiwa.
Kuchomwa moto si haki, ni kunyume na Sheria.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

11. Sheria twazidhihaki, Kwa tuhuma twasulubu.
Uchunguzi hatutaki, Twauwa na kuadhibu.
Twavunja utu na haki, Huu si Ustaarabu.
Tuungane tuzipinge, Adhabu za kikatili.

Said Rashid Hassan
ZLSC – PEMBA.

# Tanzania Bado Haijafuta Adhabu ya Kifo

**KAMISHNA** wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania, Bwana Zahor Khamis amesisitiza kwamba Tanzania na Zanzibar bado hazijafuta adhabu ya kifo katika vitabu vya sheria.

Akifungua maadhimisho ya Siku ya Adhabu ya Kifo Oktoba 10, mwaka huu katika ukumbi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) Migombani, alisema sheria za uhalifu za Zanzibar na Tanzania zinatambua adhabu ya kifo.

Alisema vipo vifungu katika hizo vinatoa adhabu ya kifo kwa baadhi ya makosa kwa mfano mauaji.

Ijapokuwa adhabu ya kifo haitekelezwi kwa muda mrefu lakini alisema Kamishna Zahor kwamba Mahkama Kuu ya Tanzania na Zanzibar zinaendelea kutoa adhabu ya kifo.

"Kutotekelezwa adhabu ya kifo haina maana kwamba adhabu hiyo imefutwa katika vitabu vya sheria. Ipo pale pale," alisema.

Alisema Tanzania inapokea shinikizo kutoka katika sehemu tofauti kufuta adhabu lakini hakuna utekelezaji uliofanyika mpaka sasa.

Baadhi ya washiriki katika maadhimisho ya Siku ya Adhabu ya Kifo walitofautina misimamo yao kuhusu utekelezaji wa adhabu ya kifo.

Walijenga hoja kwa kuzingatia imani za dini walisisitiza adhabu ya kifo isifutwe katika vitabu vya sheria.

Hata hivyo, washiriki wengine walisema adhabu ya kifo haipaswi kutumika na mbadala wake adhabu iwe kifungo cha maisha ili watu wapate kuyajutia makosa yao.



*Mgeni Rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Adhabu ya Kifo Duniani, oktoba 10,2012, Mheshimiwa Zahor Khamis,Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora akitoa hotuba yake katika Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).*

# Profesa Haroub Othman akumbukwa Pemba

Inatoka Uk. 20

Vile vile, marehemu Profesa Haroub alipenda moyo wa kujitolea katika kuwatumikia watu bila ya kuweka tamaa ya fedha mbele. Alikuwa tayari kufanya kazi bila ya malipo ilimradi jamii inafaidika.

Katika taaluma, Profesa Haroub alitoa mchango mkubwa ikiwemo kuandika na kuhariri vitabu, kusimamia machapisho ya kitaaluma katika nyanja tofauti.

Marehemu alizikwa katika kijiji cha Chuini, Wilaya ya Magharibi Unguja, ameacha mjane na mtoto mmoja.



*Marehemu Profesa Haroub Othman*

Inatoka Uk. 20

Sheria zilizopitishwa na BLW na Rais wa Zanzibar kutia saini ni hizi zifuatazo:

| NA. | JINA LA SHERIA: | NAMBA YA SHERIA |
|---|---|---|
| 1. | An Act to establish the Zanzibar Anti-Corruption and Economic Crimes Authority, its functions, powers and other matters connected therewith. | Sheria Namba 1 ya 2012 |
| 2. | An Act to repeal the specified State Leaders Retirement Benefit Act no. 4 of 1988 and Political Leaders Act, No. 6 of 1994 and to make provisions for the Grant of Retirement Benefits and Services to Political Leaders upon retirement from service in a political office and other matters connected therewith. | Sheria Namba 2 ya 2012 |
| 3. | An Act to Repeal the Zanzibar Planning Commission Act No. 5 of 1989 and enact new law to provide for the operation of the Zanzibar Planning Commission, its functions, powers and other matters connected thereto. | Sheria Namba 3 ya 2012 |
| 4. | An Act to establish Zanzibar Constituency Development Fund and other related matters. | Sheria Namba 4 ya 2012 |
| 5. | An Act to amend the Public Service Act, No. 2 of 2011 | Sheria Namba 5 ya 2012 |
| 6. | An Act to establish Zanzibar Educational Measurement and Evaluation Council and other related matters. | Sheria Namba 6 ya 2012 |
| 7. | An Act to amend the Zanzibar Tourism Act, No. 6 of 2009. | Sheria Namba 7 ya 2012 |
| 8. | An Act to establish the Zanzibar Agricultural Research Institute and other matters connected therewith. | Sheria Namba 8 ya 2012 |
| 9. | An Act to impose and alter certain taxes and duties and to amend certain written financial and tax laws relating to collection and management of Public Revenues and other related matters. | Sheria Namba 9 ya 2012 |
| 10 | An Act to appropriate the sum of six hundred and fourty eight billion, nine hundred and fourty three million, seven hundred and ninty eight thousand shillings our of the consolidated fund to the service of the year ending on the thirtieth day of june, two thousand and thirteen, to Authorise the reallocation of certain appropriation and to provide for matters incidental thereto and connected therewith. | Sheria Namba 10 ya 2012 |
| 11. | An Act to provide for protection and Management of Public and Environmental health risks and related matters. | Sheria Namba 11 ya 2012 |
| 12. | An Act to provide for the registration of business entity and other matters related thereto. | Sheria Namba 12 ya 2012 |
| 13. | An Act to establish the Zanzibar Business and Property Registration Agency and other matters related thereto. | Sheria Namba 13 ya 2012 |
| 14. | An Act to amend the Registration of Zanzibar's Resident Act No. 7 of 2005 and other related matters. | Sheria Namba 14 ya 2012 |
| 15. | An Act to provide for Registration and control of Public and Environmental Health Practitioners and establish a council for Public and Environmental health Practitioners and any other matter connected and incidental hereto. | Sheria Namba 15 ya 2012 |

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar


# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki Iwe shauku

Toleo Na. 012 | Jarida la kila miezi mitatu | Oktoba - Disemba, 2012

## Profesa Haroub Othman Akumbukwa Pemba



*Marehemu Profesa Haroub Othman*

**WANATAALUMA** na wanajamii walioshiriki katika kongamano la wasaidizi wa sheria lililofanyika Pemba walimuelezea marehemu Profesa Haroub Miraji Othman aliyefariki dunia Juni 28, 2009 kuwa alikuwa kigezo cha jamii.

"Marehemu Profesa Haroub alikuwa mpole, anayesikiliza matatizo ya watu na kuwapa ushauri, alikuwa akiwaheshimu wakubwa na wadogo na alikuwa akifuata misingi ya sheria," walisema walioshiriki katika kongamano hilo lililofanyika katika ukumbi wa Zanzibar Social Security Fund (ZSSF).

Washiriki wa kongamano hilo lililohudhuriwa na aliyekuwa mke wake Profesa Saida, mtoto wake Tahir, ndugu zake na wageni waalikwa kutoka Tanzania Bara na Kenya walisema marehemu Profesa Haroub alipenda kutetea haki za wanyonge.

Walisema marehemu Profesa alikuwa akiumia na kusikitika mno alipokuwa akisikia haki za wanyonge zimekiukwa kwa visingizio tofauti.

Kutokana na uonevu dhidi ya wanyonge, marehemu Profesa Haroub alianzisha Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) ili kutoa msaada wa bure wa sheria kwa wasiokuwa na uwezo wa kuajiri wakili kuwatetea haki zao Mahkamani.

Ilielezwa kwamba marehemu Profesa Haroub alikuwa mstari wa mbele kutoa kauli mbali mbali kupinga vitendo vya uonevu unaofanywa na watu katika jamii au taasisi za serikali.

Inaendelea Uk. 19



*Profesa Saida Othman Mjane wa Marehemu Profesa Haroub Othman watatu kutoka kushoto akisikiliza maoni ya watu mbalimbali walioelezea mchango wa marehemu Profesa Haroub katika jamii.*

## BLW Yapitisha Sheria 15 Mwaka 2012

**BARAZA** la Wawakilishi Zanzibar (BLW) limepitisha jumla ya Sheria 15 katika vikao vyake vinne vilivyofanyika katika mwaka 2012. Kawaida vikao vya BLW hufanyika kila baada ya miezi mitatu.

Afisi ya Katibu wa BLW imethibitisha kwamba sheria zote 15 zilizopitishwa na Baraza zimeshatiwa saini na Rais wa Zanzibar.

Kifungu cha 78 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kimeipa nguvu BLW kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, nguvu za kutunga sheria katika BLW itakuwa kupitisha Miswada.

Aidha, Kifungu hicho kinaeleza kwamba wakati mswada umepitishwa na BLW, Spika ataupeleka mswada huo kwa Rais ndani ya siku thelathini kupata kibali chake.

Kifungu cha 63 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinasema kwamba BLW litakuwa na sehemu mbili, Rais wa Zanzibar kwa upande mmoja na Wawakilishi kwa upande wa pili.

Inaendelea Uk. 19